Jinsi Ya Kufanya Kazi Na Mungu

Na

Ellis P. Forsman

(How To Work With God)

Jinsi Ya Kufanya Kazi Na Mungu

Na

Ellis P. Forsman

Oktobaa 12, 2011

Jinsi Ya Kufanya Kazi Na Mungu

2 Kor.6:1

2 Kor. 6:1, "*Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msipokee neema ya Mungu bure.*"

Labda umewahi kuona ishara au matangazo kama haya:

- "Nahodha wanatafuta watu wachache wazuri."
- "Waombaji wenye sifa."

"Lazima waweze kushughulika na watu…"

Kila taasisi wanahitaji watu bora ili waweze kuzifanyia kazi:

Mahusiano ya mwanadamu inakuwa ndo sababu ya kupewa kazi. Swali la msingi ni: "Je anaendeleaje na watu.?"

Wengi huamini kwamba hii ni mhumu hata kuliko shahada ya chuo.

Nilifanya kazi na watu waliokuwa na "akili" katika kuifahamu kazi yao lakini hawakuwa na maelewano mazuri na watu wengine. Kimsingi hawakudumu.

Wakati mkwe wangu alipoomba kazi katika kampuni ya Boeng, msimamizi wa eneo hilo alipokuwa akimuongelea kwa msimamizi mkuu alisema, "…na hakika ni mwanadamu."; akimanisha kwamba alikuwa na mawasiliano mazuri katika mambo mengine nje ya eneo lake la masomo.

Mungu anawahitaji watu:

Ezekieli 22:30, "*Nami nikatafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeza boma na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka kwa ajili ya nchi, nisije nikaiharibu lakini sikuona mtu.*'

Mungu hakumpata mtu wa kufanya naye kazi! Ni huzuni kiasi gani. Yeye, Mungu, "bado anamtafuta mtu mmoja." – Micaiah:

1 Fal. 22:1-40, "*Wakakaa miaka mitatu pasipo vita kati ya Shamu na Israeli. Ikawa mwaka wa tatu Yehoshafati mfalme wa Yuda akamshukia mfalme wa Israeli. Mfalme wa Israeli akawaambia watumishi wake, Je! Hamjui ya kuwa Ramoth-Gileadi ni yetu? Nasi tumenyamaza tusiitwae mkononi mwa mfalme wa Shamu? Akamwambia Yehoshafati, Je! Utakwenda nami tupigane na Ramoth-gileadi? Yehoshafati akamwambia mfalme wa Israeli, mimi ni kama wewe,*

na watu wangu ni kama watu wako na farasi zangu ni kama farasi zako. Yehoshafati akamwambia mfalme wa Israeli, Uulize leo nakusihi kwa neno la BWANA. Ndipo mfalme wa

Israeli akawakusanya pamoja manabii kama watu mia nne. Akawambia je niende juu ya Ramoth- Gileadi kuupiga vita au ninyamaze? Wakasema kwea; kwa kuwa BWANA atautia mkononi mwa mfalme. Lakini Yehoshafati akasema, Je! Hayupo hapa nabii wa BWANA tena, ili tumwulize yeye? Mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati, yupo mtu mmoja ambaye tungeweza kumwuliza BWANA kwa yeye, yaani Mikaya mwana wa Imla; lakini namchukia; kwa kuwa hanibashirii mema, ila mabaya. Yehoshafati akasema, La! Mfalme asiseme hivi. Ndipo mfalme wa Israeli akamwita akida, akamwambia mlete hima Mikaya mwana wa Imla. Basi mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa Yuda walikuwa wakikaa kila mtu katika kiti chake cha enzi, wamevaa mavazi yao katika sakafu langoni pa Samaria; na manabii wote wakafanya unabii mbele yao. Na Zedekia mwana wa Kenaana akajifanyia pembe za chuma, akasema BWANA asema hivi, kwa hizo utawasukuma Washami hata waharibike. Na manabii wote wakasema hivyo kwa unabii, wakisema kwea Ramoth-Gileadi ukafanikiwe kwa kuwa BWANA atautia mkononi mwa mfalme. Na yule mjumbe aliyekwenda kumwita Mikaya, akamwambia akasema angalia sana, maneno ya manabii kwa kinywa kimoja husema mema kwa mfalme; neno lako na liwe, nakusihi kama neno la mmojawapo wao, ukaseme mema. Mikaya akasema kama BWANA aishivyo, neno lile BWANA aniambialo, ndilo nitakalolinenaa. Na alipokuja kwa mfalme, mfalme alimwambia, je! Mikaya tuende Ramoth-Gileadi kupiga vita au tunyamaze? Akamwambia kweya ufanikiwe; kwa kuwa BWANA atautia mkononi mwa mfalme. Mfalme akamwambia, mara ngapi nikuapishe usiniambie neno ila yaliyo kweli, kwa jina la BWANA? akasema naliwaona Waisraeli wote wametawanyika milimani kama kondoo wasio na wachungaji. BWANA akasema hawa hawana bwana; na warudi kila mtu nyumbani kwake kwa amani. Mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati, Je! Sikukwambia hatanibashiria mema, ila mabaya? Mikaya akasema, sikia basi neno la BWANA; nalimwona BWANA ameketi katika kiti chake cha enzi, na jeshi lote la mbinguni wamesimama upande wa mkono wake wa kuume na wa kushoto. BWANA akasema, ni nani atakayemdanganya Ahabu, ili akwee Ramoth-Gileadi akaanguke? Basi huyu akasema hivi; na huyu hivi. Akatoka pepo, akasimama mbele za BWANA, akasema, mimi nitamdanganya. BWANA akamwambia, jinsi gani? Akasema nitaondoka na kuwa pepo wa uongo kinywani mwa manabii wake wote. Akasema utamdanganya na kudiriki pia; ondoka ukafanye hivyo. Basi angalia BWANA ametia pepo wa uongo kinywani mwa manabii hawa wote; naye BWANA amenena mabaya juu yako. Ndipo akakaribia Zedekia, mwana wa Kenaana akampiga Mikaya kofi la shavu, akasema, roho ya BWANA alitokaje kwangu ili aseme wewe? Mikaya akamwambia, angalia utaona siku ile utakapoingia katika chumba cha ndani ili ajifiche. Mfalme wa Israeli akasema mchukueni Mikaya, mkamrudishe kwa amoni mkuu wa mji na kwa Yoashi mwana wa mfalme; mkaseme mfalme asema hivi, mtieni mtu huyu gerezani mkamlishe kwa chakula cha shida, na maji ya shida, hata nitakaporudi kwa amani. Mikaya akasema, ukirudi kabisa kwa amani, BWANA hakusema kwa mimi. Akasema sikieni enyi watu wote. Basi mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa Yuda wakakwea mpaka Ramoth-Gileadi. Mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati, nitajibadilisha na kuingia vitani; lakini

wewe uvae mavazi yako. Mfalme wa Israeli akajibadilisha akaingia vitani. Basi mfalme wa Shamu alikuwa amewaamuru wakuu wa magari yake thelathini na wawili, akisema msipigane na mdogo wala mkuu, ila na mfalme wa Israeli peke yake. Ikawa wakuu wa magari walipomwona Yehoshafati, wakasema, huyo ndiye mfalme wa Israeli wakageuka juu yake ili wapigane naye; naye Yehoshafati akapiga ukulele. Ikawa wakuu wa magari walipoona ya kuwa siye mfalme wa Israeli, wakageuka nyuma wasimfuate. Mtu mmoja akavuta upinde kwa kubahatisha, akampiga mfalme wa Israeli mahali pa kuungana mavazi yake ya chuma; kwa hiyo akamwambia mwendesha gari lake, geuza mkono wako unichukue kutoka katika majeshi; kwa kuwa nimejeruhiwa sana. Pigano likazidi siku ile; mfalme akategemezwa garini mwake, kinyume cha Washami, hata jioni akafa; damu ikatoka katika jeraha yake ndani ya gari. Ikapigwa mbiu jeshini, jua likichwa, kusema kila mtu aende mjini kwake, na kila mtu shambani kwake. Hivyo akafa mfalme akachukuliwa Samaria, wakamzika mfalme huko Samaria. Wakaliosha gari penye birika la Samaria, na mbwa wakaramba damu yake; (basi ndipo walipooga makahaba); sawasawa na neno la BWANA alilolinena. Naa mambo yote ya ahabu yaliyosalia, na yote aliyoyafanya, na nyumba ya pembe aliyoijenga, na miji yote aliyoijenga, je! Hayakuandikwa katika kitabu cha tarehe cha wafalme wa Israeli? Basi Ahabu akalala na baba zake; na Ahazia mwanawe akatawala mahali pale."

Kwa nini Mungu anawahitaji watu wema?

Ana kazi zenye mipaka katika vyombo vya udongo.

- Rum. 1:14-16, "*Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekina na wasio na hekina. Kwa hiyo, kwa upande wangu, <u>mimi ni tayari kuihubiri Injili</u> hata na kwenu mnaokaa Rumi. Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni <u>uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye</u>, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.*"
- 2 Kor. 4: , "*Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu.*"

Hivyo, siyo tu kwamba mwanadamu yeyote atafanya. Mungu hatafuti viwango vya kiroho vya kutokuajiriwa bali anaangalia wanajitolea. Kazi yake inachangamoto na inahitaji watenda kazi wanaojitolea.

Katika somo hili tunaenda kujifunza baadhi ya ukweli kuhusu kufanya kazi na Mungu.

Mungu anahitaji watu watakaofanya naye kazi

Mtu anaweza kukubalika kuhusu mambo mengi:

Anaweza aakawa na ujuzi wa neno la Mungu, Kiyahudi, Kiyunani, kisaikolojia, mifumo, n.k., na bado asiwe tayari kufanya kazi na Mungu. Kwa nini? Hajui ni kwa nini.

Biblia inaiweka wazi kwamba tunapaswa kufanya kazi na Mungu:

- 2 Kor. 6:1, "*Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msipokee neema ya Mungu bure*."
    - 1 Kor. 3:9, "*Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu.*"

Mmoja alipandikiza, mwingine akatia maji, na Mungu akakuza. 1 Kor. 3:6-8, "*mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo apandae si kitu, wala atiaye maji, bali Mungu akuzaye.*"

Nabii Yona ni mfano mzuri wa mtu ambaye hakutaka kufanya kazi na Mungu (kwa sharti la Mungu). Mungu alimpa Yoha agizo la kwenda na kuhubiri toba Ninawi.

Yoha 1:1-4, "*Basi neno la BWANA lilimjia Yona mwana wa Amitai, kusema, ondoka, uende Ninawi mji ule mkubwa ukapige kelele juu yake; kwa maana uovu wao umepanda juu mbele za Mungu. Lakini Yona akaondoka akimbilie Tarshishi apate kujiepusha na uso wa BWANA; akatelemka hata Yafa, akaona merikebu inayokwenda Tarshishi; basi akatoa nauli akapanda merikebuni, aende pamoja nao Tarshishi, ajiepushe na uso wa BWANA. Lakini BWANA alituma upepo mkuu baharini, ikawa tufani kibwa baharini, hata merikebu ikawa karibu na kuvunjika.*"

Yona alikimbia wajibu wake.

Inahitaji maandalizi kufanya kazi na Mungu:

- Mitume walifundishwa kwa miaka 31/2 na Bwana.
- Roho Mtakatifu aliwajia kukamilisha kazi ya kufundisha iliyoanzishwa na Yesu.
- Kazi yetu, pia, ni kuwafundisha watu waaminifu. 2 Tim. 2:2, "*Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha wengine.*"

Mungu anahitaji watu wanaofanya kile wanachohubiri.

Uaminifu ni changamoto katika wakati wetu:

Tunazongwa na watu wachafu wanaojaribu kutumia vyombo vya habari ili kututawala.

- Wanasiasa wengi husema kile ambacho watu wanataka kusikia.
- Maongezi ya wazi ni kwa ajili ya pesa au starehe.

Uaminifu hukosekana katika dini:

Hutambui kama mtumiaji wa madawa ni baba mzuri, analipa angara zake, au ni mwema. Unamhitaji tu ajaze mahitaji yako.

Ujumbe wa Injili, hativyo, imechanganywa na anayetoa. Huwezi kutenganisha ujumbe na mtoa ujumbe.

Kama mhubiri haishi kwa kile anachohubiri, watu hawawezi kuamini kile anachohubiri.

Mtoa ujumbe hawezi kuhubiri dhabihu wakati “anaishi maisha machafu.”

Mtoa ujumbe hawezi kuhubiri fanya, wakati hafanyi yeye mwenyewe. Hawezi kuhubiri nenda, na yeye haendi mwenye.

Mungu anahitaji watu wanataka kuwa kama Bwana wao

Alikuwa mtumishi wa wote.

Fil. 2:5-8, “*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya utumwa, akawa ana mfaano wa mwanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu , alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.*”

Alifundisha kuhusu kuwa mtumishi.

Mat. 10:24-26, “*Mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumwa hampiti bwana wake. Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake. Ikiwa wamemwita mwenye nyumba Beelzebuli, je! Si zaidi wale walio wa nyumbani mwake? Basi, msiwaogope kwa maana hakuna neno lililositirika, ambalo halitafunuliwa; wala lililofichwa, ambalo halitajulikana.*”

Alikuja kuwa mtumishi.

Marko 10: 45, “*Kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.*”

Mhubiri wa Injili anatakiwa kushikilia neno la Mungu sawasawa na uwezo ambao Mungu amempa. 1 Pet. 4:11, “*Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.*”

Hii inamanisha kuwa na nia njema. Mit. 23:7, “*Maana aonavyo nafsini mwake ndivyo alivyo. Akuambia, haya kula, kunywa; lakini moyo wako hauwi pamoja nawe.*”

Jinsi ya kufanya kazi na Mungu

(Kuna mambo mengi inayojumuishwa katika kufanya kazi na Mungu. Kuma mambo kadhaa ambazo lazima zifuate kama unataka kufanya kazi na Mungu:)

Unafanya kazi na Mungu kwa kumjua Mungu. Hatupaswi kuwa wageni.

Yohana 17: 3, "*Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.*"

Unafanya kazi na Mungu kwa kumsikiliza yeye. Zab. 85:8, "*Na nisikie atakavyosema Mungu BWANA, maana atawaambia watu wake amani, naam, na wataauwa wake pia, bali wasiurudie upambavu tena.*"

Unafanya kazi na Mungu kwa kufikiria kuhusu fikira zake. Isa. 55:6-11, "*Mtafuteni BWANA maadamu anapatikana, mwiteni maadaamu yu karibu; mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa. Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA. kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazzo yangu kuliko mawazo yenu. Maana kama vile mvua ishukavyo, na theluji kutoka mbinguni, wala hairudi huko; bali huinywesha ardhi, na kuizalisha na kuichipuza, ikampa mtu apandaye mbegu, na mtu aalaye chakula; ndivyo litakavyokuwa neno langu litokalo katika kinywa change; halitanirudia bure bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma.*"

Unafanya kazi na Mungu kwa kutii maagizo yake.

- Luka 6:46, "*Na kwa nini mnaniita Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?*"
- Heb. 5:8-9, "*Na ingawa ni Mwana alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*"

Unafanya kazi na Mungu kwa kuliamini neno lake.

- Yohana 8:32, "*Tena mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru.*"
- Yohana 8:36, "*Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli.*"

Unafanya kazi na Mungu kwa kuwa mtakatifu katika maisha yako. 1 Pet. 1:15, "*Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote.*"

Unafakazi na Mungu kwa kutii vipaumbele vyake. Mt. 6:33, "*Bali ufuateni sana ufalme wake, na haki yake na hayo yote mtazidishiwa.*"

Unafanya kazi na Mungu kwa kutafuta mapenzi yake katika vitu vyote. Yakobo 4:15, "*Badala ya kusema, Bwana akipenda, tutakuwa hai na kufanya hivi au hivi.*"

Unafanya kazi na Mungu kwa kuishi na kufanya kazi kwa imani. Heb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"

Unafanya kazi na Mungu kwa kutotembea kwa kufuata mwili. Rum. 8:1-12, "*Sasa basi hakuna hukumu yaa adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa*

uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi tusionenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho. Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kutii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali waifuata roho. Lakini mtu yeyote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake. Na Kristo akiwa ndani yenu, mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi; bali roho yenu I hai, kwa sababu ya haki. Lakini ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu. Basi kama ni hivyo ndugu tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili."

Hitimisho

Mungu anawahitaji wanaume (na wanawake) kufanya kazi pamoja naye. Mahitaji yake ni muhimu kuliko mahitaji ya mtu mwingine awaye yote ulimwenguni. Kazi yake, kupitia mwanadamu, ni wokovu war oho.

Mungu anawahitaaji watu kama Filipo. Mdo. 8:26-40, "*Malaika wa Bwana akasema na Filipo akamwambia ondoka uende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza nayo ni jangwa. Naye akaondoka akaenda mara akamwona mtu wa Kushi towashi mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo sogea karibu na gari hili ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena je yamekuelea haya haya unayosoma? Akasema nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, na kama vile mwanakondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. yule towashi akamjibu Filipo, akasema nakuomba nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake naye akianza kwa andiko lilo hilo akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani wakafika mahali penye maji, yule towashi akasema tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? [Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akanena naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu] akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi naye akambatiza. Kisha walipopanda*

kutoka majini Roho wa Bwana akamnyakua Filipo yule towashi asimwone tena basi alikwenda zake akifurahi. Lakini Filipo akaonekana katika Azoto, na alipokuwa akipita akahubiri Injili katika miji yote, hata akafika Kaisaria."

Mungu anawahitaji watu walio na miguu mizuri. Rum. 10:13-17, "*Kwa kuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikiaje yeye wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema. Lakini si wote walioitii ile habari njema. Kwa maana Isaya asema Bwana, ni nani aliyeziamini habari zetu? basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Je unafanya kazi na Mungu? Ni lazima uwe Mkristo ili uweze kumfanyia kazi.

Ni jinsi gani mtu anafanyika Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu, umri sawa na wa kwangu alikuwa haamini kuwa Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye ana kwa ana kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ili kuwa ni nzuri. Lakini ili kuwa upande ambao ni salama, labda anaweza kwenda kanisani, na kama akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri na kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "mambo haya hayafanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umwamini yeye kwa moyo wako wote, la sivyo huwezi kumpendeza."
- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Matend. 11:18, "..... *Mungu amewapa pia mataifa toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa una lala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani humu!" unachukuwa simu na taratibu unawapigia polisi, ukiwambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani ya nyumba yako. Kidogo, unawasikia wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadilisha maisha yake ili kwamba asiibe tena. Ni badiliko la akili linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Warumi 10:9-10*, "Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hatakupata haki, na kwa kinywa hukiri hatakupata wokovu."*

Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu. Kumbuka kwamba katika somo hilo hapo juu imani (kuamini), toba na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" humaanisha kuelekea kitu fulani; si kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki inapatikana, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote,

"*Lakini Yohana alitakakumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa alipanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa mpendwa wangu ninayependezwa naye*." (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi ya kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia alisema "*imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni makabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, ulisema ubatizo ni kwa ajili ya nini? *"Kwa ajili ya ondoleo la dhambi."* Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. *"Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ukabatizwe uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16).

Ubatizo ni agizo lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Hivyo mnazikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kama vile Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale ni lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaungana kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* (Rum. 6:3-6).

Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa njia ya ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi “kunyunyiza. Andiko hapo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatuendi makaburini na kuchukua udongo kidogo na kuweka juu ya mwili wa marehemu.

Kama hujafanyika mshiriki wa kanisa la Kristo, kwa nini usizingatie leo?